# ‘Hakuna uhusiano uchimbaji madini, upungufu samaki’

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kirusa, amesema hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uchimbaji madini na upungufu wa samaki katika miti na maziwa.

Alitoa ufafanuzi huo bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Jumbe.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji uchimbaji wa madini kando ya mito na maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki.

Akiijibu swali hilo, Dk.Kirusa alisema uchimbaji wa madini umegawanyika katika aina kuu mbili, uchimbaji juu ya ardhi na ule wa chini ya ardhi.

“Sheria ya Madini Sura 123 ambayo hairuhusu uchimbaji wa madini katika vyanzo vya mito na maziwa na endapo shughuli za uchimbaji zitafanyika kando ya mto au maziwa zitafanyika umbali wa mita 60 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 20 ya mwaka 2004,”alisema.

Aidha, alisema kabla ya shughuli za uchimbaji wa madini kufanyika katika eneo husika tathmini ya mazingira hufanyika na kutathmini athari za kimazingira ikiwamo viumbe hai pamoja vyanzo vya maji.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema utafiti uliofanyika Aprili mwaka 2018, Marekani ilionyesha kuwa sehemu zenye machimbo ya makaa ya mawe karibu na mito kuna upungufu wa viumbe wa majini kwa asilimia 53 ikiwamo samaki.

“Je, sisi serikali yetu imefanya utafiti huo na kuja na majibu haya? Sasa hivi tunaanza kuchimba makaa ya mawe pale Kiwira, Mto Kiwira na Songwe imeathiriwa kwa namna hiyo, je, ni hatua gani zinazochukuliwa na serikali ili kusiendelee kupatikana kwa athari hizo,”alihoji.

Dk. Kiruswa akijibu maswali hayo, alisema Tanzania haina uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya mito au maziwa ambayo yanasababisha athari hiyo.

Hivyo, alimhakikishia mbunge huyo kuwa katika eneo la machimbo ya makaa ya mawe Kiwira, tahadhari zote za mazingira zimechukuliwa na hakuna athari.




Habari zote: Augusta Njoji, DODOMA

hizo kupatikana wakati wowote inapohitajika," alisema.

Chande alisema fedha za Mfuko wa Jimbo kwa majimbo ya

tolewa kwa ajili ya majimbo ya Zanzibar.

# 'Hakuna uhusiano uchimbaji madini, upungufu wa samaki'

NAIBU Waziri wa Madini, Dk Steven Kiruswa amesema hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uchimbaji wa madini na upungufu wa samaki katika mito na maziwa.

Dk Kiruswa alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Kyela, Ally Mlaghila (CCM).

Mlaghila alitaka kujua kama uchimbaji wa madini kando ya mito na maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki. Dk Kiruswa alisema uchimbaji wa madini umegawanyika katika aina kuu mbili, uchimbaji juu ya ardhi na wa chini ya ardhi.

Alisema uchimbaji huo unazingatia Sheria ya Madini Sura ya 123 ambayo hairuhusu uchimbaji wa madini katika vyanzo vya mito na maziwa.

Alisema shughuli za uchimbaji zinatakiwa kufanyika umbali wa mita 60 kando ya mto au ziwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004.

Aidha, alisema kabla ya shughuli za uchimbaji wa madini kufanyika katika eneo fulani, tathmini ya mazingira hufanyika juu ya athari za kimazingira ikiwamo viumbe hai pamoja na vyanzo vya maji.

# ‘Fugeni viumbe maji mnyanyue uchumi wenu’

**Na Sifa Lubasi, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk Mashimba Ndaki, amewahimiza Watanzania kujikita katika ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji ili kujikomboa kiuchumi.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati wa uzinduzi wa vitabu vyenye miongozo ya ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji. Vitabu hivyo vimeelezwa kwamba vinalenga kusaidia wananchi kufanya ufugaji wa kisasa.

Akifafanua zaidi, Dk Ndaki alisema ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji ni muhimu kwa taifa kwa sababu ni shughuli ya kiuchumi inayokuza kipato, kutengeneza ajira na kuboresha lishe ya wananchi.



Alisema kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 kuna wafugaji zaidi ya milioni nne wanaofuga kuku kuanzia 10 na kuendelea, ambayo ni sawa na asilimia 55.3 ya wafugaji wote.

Alifafanua kuwa uzinduzi wa miongozo hiyo umekuja wakati mwafaka na kuitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kujipanga vyema kuzisambaza katika kila ngazi kuanzia ngazi ya halmashauri hadi kata ili iweze kuwafikia walengwa.

“Tunatakiwa kuona ni namna gani tutahamasisha wafugaji ambao ni wananchi wetu ili waingie kwa nguvu kwenye ufugaji wa sungura kwa sababu ni chanzo cha lishe lakini pia ni chanzo cha kipato kizuri,” alisema Dk Ndaki.

Alitaka wataalamu kuhakikisha kwamba miongozo hiyo haikai katika makabati bali kupelekwa kwa wananchi ili kufaidisha ufugaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya USAID/Lishe Endelevu, Dk Joyceline Kaganda alisema Lishe Endelevu ni mradi wa miaka mitano unaofadhiliwa na USAID na kutekelezwa na Save the Children International na washirika wake.

Mradi huo unatekelezwa katika mikoa minne ya Dodoma, Morogoro, Iringa na Rukwa ambapo ulianza Oktoba 2018 hadi Septemba 2023.

Dk Kaganda alisema katika utekelezaji huo, Lishe Endelevu kwa kushirikiana na MLF imeweza kuandaa miongozo ya mafunzo na uzalishaji kwa ajili ya matumizi ya wakulima, maofisa ugani na wadau wengine wa mnyororo wa thamani.

Alisema hadi sasa watumishi 290 wa halmashauri (254 mifugo na 46 Ukuzaji viumbe maji) wamepata mafunzo katika maeneo mbalimbali, kama vile uzalishaji kwa ujumla, usimamizi wa bwawa, ujenzi wa bwawa, uundaji na uzalishaji wa malisho pamoja na uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

CS CamScanner

wa 30 wa Wanahisa wa benki hiyo. Wa pili kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi na maofisa wengine. (Picha na TCB).

Tanzania ambao kupitia ushirikiano wao wameweza kujitanua nchi nzima.

# Wapongeza Tanzania inavyokuza teknolojia ya ngozi

**Na Abela Msikula, Mwanza**

MKUFUNZI kutoka chuo cha ufundi cha Kisumu National Polytechnic cha nchini Kenya, Mariam Cassim, amepongeza juhudi zinazofanywa na serikali ya Tanzania katika kukuza teknolojia ya ngozi, hatua itakayowasaidia vijana wengi kujiajiri.

Mkufunzi huyo na baadhi ya wanafunzi wake wapo Tanzania kwa ajili ya kujifunza uchakataji na utengenezaji bidhaa za ngozi katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Kampasi ya Mwanza.

Ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP), ambapo vyuo hivyo viwili vimebadilishana wanafunzi, kwa ajili ya kila upande kujifunza kile ambacho hakifundishwi nchini au chuoni kwao.

"Sisi tumekuja kujifunza utengenezaji wa bidhaa za ngozi, ikiwemo viatu, masomo ambayo chuo chetu hakifundishi. Ni hatua muhimu kwani nchini kwetu mifugo ya kutupatia malighafi ni mingi lakini hatuna ujuzi hata kidogo wa kuchakata ngozi. Matokeo ya kukosa ujuzi ni matumizi yasiyofaa ya ngozi," aliliambia gazeti hili jana.

Aliongeza kwamba kikubwa kinachofanyika katika chuo chao ni mafunzo ya ushonaji wa mavazi, na baada ya kupata ujuzi wa kuchakata ngozi watahakikisha kila vazi linalotengenezwa linakua na kiatu chake pamoja na bidhaa zingine za ngozi, ikiwemo mikoba na mikanda.

Alipongeza pia uwepo wa walimu wenye ujuzi DIT katika kuchakata ngozi, ambao wamewasaidia wanafunzi hao wageni kujifunza mambo mengi ndani ya muda mfupi.

Kwa niaba ya wanafunzi wenzake wa Kisumu National Polytechnic, Marion Obondi alisema mafunzo hayo ya vitendo kwa siku 21 kuanzia Juni 10, yatawapatia hamasa ya kujiajiri baada ya masomo na kuhimiza matumizi bora ya ngozi nchini mwao.

Alisema tayari wamemudu kutengeneza michoro ya viatu pamoja na kuvishona.

"Tunaenda kueneza ujuzi huu kwa wanafunzi wenzetu na wanajamii kwa ujumla ili tuweze kujiajiri, hatua ambapo pia itapunguza gharama za bidhaa za ngozi nchini kwetu," alisema.

Mratibu wa EASTRIP wa DIT, Issa Mwangosi alisema kubadilishana ujuzi si tu kwa wanafunzi bali hata walimu ili kukuza teknolojia na thamani ya ngozi ndani na nje ya nchi zinazonufaika na mradi huo, ambazo ni Tanzania, Kenya na Ethiopia.

IA MAJIBU
NKONDO



i kupokea taarifa na kuitunza katika seva

## tika maandishi

Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alitoa kauli hiyo baada ya Mbunge wa Mtoni (CCM) Abdul-Hafar Idrissa Juma, kuuliza ni lini majimbo ya Zanzibar yatapata fedha za mfuko wa jimbo kwa wakati.

Akijibu swali hilo, Naibu waziri Chande alisema fedha za mfuko wa jimbo kwenda majimbo ya Zanzibar hupelekwa kwa wakati na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha ambapo fedha hizo uhamishwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, alisema katika mwaka 2021/22 fedha za mfuko sh. bilioni 1.4 zimeshatolewa kwa ajili ya majimbo ya Zanzibar.



ndisha hadhi mapori tengefu,

## iboreshwa

awe na ujenzi wa maboksi kalavati ' alieleza.

na serikali itaendelea kuboresha nbinu ya barabara za halmashauri ingana na upatikanaji rasilimali

**Mbunge**

**ULIZA**

*kali itatenga fedha kutengeneza a ya Wino hadi Ifinga ambayo a masika haipitiki.*

# Uchimbaji madini kando ya mito hausababishi upungufu wa samaki

SERIKALI imeeleza hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa uchimbaji wa madini na upungufu wa samaki katika mito na maziwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Madini, Stephen Kiruswa, wakati akijibu swali la Mbunge wa Kyela (CCM) Ally Mlaghila ambaye alihoji kama kweli uchimbaji madini kando ya mito na maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema uchimbaji wa madini umegawanyika katika aina kuu mbili ambazo ni uchimbaji juu ya ardhi na mwingine wa chini ya ardhi.

Alisema uchimbaji huo unafuata Sheria ya Madini Sura 123 ambayo hairuhusu uchimbaji madini katika vyanzo vya mito na maziwa.

"Endapo shughuli za uchimbaji zitafanyika kando ya mto au maziwa zitafanyika umbali wa mita 60 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004," alibainisha.

Alisisitiza kabla ya shughuli za uchimbaji madini kufanyika katika eneo husika, tathmini ya mazingira hufanyika na kutathmini athari zake ikiwemo viumbe hai na vyanzo vya maji.

Kwa sababu hiyo, alisema hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa uchimbaji madini na upungufu wa samaki katika mito na maziwa.

> **Endapo shughuli za uchimbaji zitafanyika kando ya mto au maziwa zitafanyika umbali wa mita 60 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004.**
>
> Naibu Waziri wa Madini, Stephen Kiruswa.

puni za uzalishaji vifaranga zilizoko nchini

a
a

a
i
l

# SUA waja na programu kulinda kuku wa kisasa

**NA LATIFA GANZEL**, *Morogoro*

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imewapongeza watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa kuanzisha programu inayolenga kuhakikisha usalama wa kuku wa kisasa ili kulinda afya za walaji.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, wizara hiyo, Profesa Hezron Nonga, alipokuwa akizindua programu ya kudhibiti ongezeko la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa kwa njia ya kinga na kanuni bora za ufugaji.

Alieleza kwamba mradi huo utasaidia kutoa majibu mengi yanayowasumbua wafugaji wa kuku wa kisasa na walaji kuhusu usalama wake, pia mbinu bora za ufugaji kwa wafugaji wa kisasa na kupunguza matumizi ya dawa yasiyo ya lazima.

Alisema taarifa za kina zinaonyesha ongezeko la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa ni kubwa hususanasa kwa sababu ya dawa za antibayotiki zinazotumika kwa kuku.

"Tunatamani kujua kuku anaposhindwa kufanya vizuri na kudumaa bandani ni sababu ya chanjo peke yake au ni kwa sababu amekosa usafi. Maana kama chakula anakula na tunaambiwa anayekula vizuri anakuwa na kinga yenye nguvu," alieleza.

Aliongeza wapo watengenzaji vya vyakula vya kuku na wazalishaji wa vifaranga wanaojisifia kuwa bora, lakini utafiti haujawahi kufanyika kujua ukweli.

"Tanzanaia tuna zaidi ya kampuni 26 za uzalishaji wa vifaranga na wengine ukivinunua wanakupa na nyongeza ya hadi robo ya vile ulivyochukua. Maana yake anajua kiwango cha vifo vya vifaranga vyake ni kikubwa, hivyo hao wa nyongeza watakusaidia kurudishia wale asilimia 40 watakaokufa."

"Wakulima wa bustani hususan mboga nao wanachukua mbolea hiyo ambayo unakuta imejaa dawa na kuweka katika bustani zao. Mboga zinafyonza dawa hiz,o kisha zinakwenda kuingia katika miili ya watumiaji na kusababisha kupata usugu wa vimelea dhidi ya dawa," alisema.

Kiongozi wa progamu hiyo, Profesa Robinson Mdegela, alisema ni ya miaka mitatu na ina miradi miwili ya kinga na matumizi ya kibiolojia kupunguza magonjwa kwa kuku na kuzuia matumizi makubwa ya dawa kwa kuku.

Mwingine unahusisha mbinu za uchakataji wa samadi ya kuku ili kulinda afya na mazingira.

CamScanner

## SOKONI



**WACHUUZI** wa mbuzi wakisubiri wateja katika eneo la Vingunguti, Dar es Salaam, jana. Mbuzi mmoja aliuzwa kati ya sh. 70,000 hadi 150,000. (Picha na Christopher Lissa).